AINA NA VIWANGO VYA KODI YA BIASHARA.

Benittotz
Member
Joined: May 24, 2018
45 51 25

ZIFAHAMU AINA ZA KODI NA VIWANGO VYAKE KWA MFANYABIASHARA MDOGO NA WA KATI.

: KODI NI NINI?

 Kodi ni mchango wa lazima kwa serikali kutoka katika malipo ya mishahara, utoaji wa huduma au uuzwaji wa bidhaaa, gharama za nyongeza katika kuhamisha mizigo au kiwango Fulani kinachokatwa katika miamala.
 Kodi ya biasha hutokana na mauzo ya mwaka au faida kulingana na ukubwa na Aina ya BIASHARA.
 Serikali inahitaji Kodi katika kutekeleza miradi ya kijamii na kuleta Maendeleo vile vile.
 Kunahitajika uwazi, usawa, gharama ndogo za ukusanyaki kodi na uchache wa Kodi hizi ili kuleta Maendeleo chanya katika jamii husika.

AINA ZA KODI ZA BIASHARA

 Presumptive tax. Kodi ya makisio hi NI kwa wafanyabiashara wadogo wasio na daftari za hesabu za fedha. Muhusika hutozwa Kodi kulingana na mauzo yake ya mwaka (annual turnover).
 Audited ta. Hi ni Aina ya kodi inayohusisha wafanyabiashara biashara wenye vitabu vya kumbukumbu za hesabu bazo hutumika kutoa tathmini ya kiwango cha kodi kinachopaswa kulipwa.

VIGEZO VYA KUZINGATIA KATIKA KODI YA
MAKISIO

 Mhusika anapaswa kuwa mkazi wa Jamuhuri ya muungano wa Tanzania. Katika upande wa Kodi ulikuwa mkazi vitu vitatu huzingatiwa zaidi

1. Lazima uwe na sehemu ya kumudu ya kuishi Na uwepo nchini katika mwaka husika wa fedha. Hapa hawamaanish lazima uwe umejenga. Sehemu ya kudumu ya makazi ni sehemu yoyote unayoishi Kama vile nyumba ya kupanda au chumba katika nyumba ya wageni ila TU wahusika wa eneo husika wawe wanatambua uwepo wako.

2. Uwe umeishi nchini kwa kipindi cha zaidi ya siku 183 au Zaid katika mwaka husika wa fedha.

3. Uwe nchini katika huo mwaka wa fedha na uwe na wastani wa kuishi nchini kwa siku zaidi ya 122 kwa kipindi Cha miaka miwili iliyopita

4. Uwe mfanyazi au afisa was serikali uliyeko nje kikazi wakati was mwaka wa fedha.

 Biashara yako iwe inaingiza chini ya Tsh 20 million kwa mwaka.
 Kipato chote kinapaswa kutokana na biashara katika mwaka husika wa fedha. Hivyo mhusika hapaswi kujihusisha na shughuli zinginezo kama vile ajira na uwekezaji.
 Mapato yake ya mwaka wa fedha yanapaswa kutokana na biashara ambazo vyanzo vyak viko ndani ya jamhuri ya muungano wa Tanzania pekee.

VIWANGO VYA KODI KATIKA MFUMO WA
MAKADIRIO

 Katika mfumo huu kiwango Cha Kodi kinachohitajika hupatikana kwa kuzingatia mauzo ya mwaka yatakayoonyeshwa katika taarifa ya
mfanya biashara. Kama taarifa hizo hasijakamilika , makadirio mazuri hufanyika na kamishina na kiwango sahihi kupatikana..
 Viwango hivyo kwa taarifa Kamili na zisizo Kamilika vimeonyeshwa Hapo chini Kama ifuatavyo.

mapato ya mwaka
Yakiwa chini ya 4,000,000.

Makadirio ya Kodi taarifa zikiwa Kamili ni;
NIL (-)
Mapato ya mwaka yakiwa zaidi ya 4,000,000 lakini ni sawa auchini ya 7,500,000.
Makadirio ya Kodi taarifa zikiwa nusu ni
TSH 150,000.
Makadirio ya Kodi taarifa zikiwa Kamili ni
3% ya kiwango kilichozidi katika 4,000,000
Mapato ya mwaka .
Kiwango kinapozidi 7,500,000 lakini NI sawa au chini ya 11,500,000.
Makadirio ya Kodi taarifa zikiwa nusu ni
TSH 318,000
Makadirio ya Kodi taarifa zikiwa Kamili ni
Tsh 135,000 +3.8% ya kiwango Cha mapato kilichozidi katika 7,500,000.
Mapato ya mwaka
Kiwango kinapozidi 11,500,000 lakini Sawa au chini ya 16,000,000.
Makadirio ya Kodi taarifa zikiwa nusu ni
Tsh 546,000.
Makadirio ya Kodi taarifa zikiwa Kamili ni
Tsh 285,000 + 4.5% ya kiwango kilichozidi katika 11,500,000.
Mapato ya mwaka
Yanapokuwa zaidi ya 16,000,000 lakini sawa au chini ya 20,000,000.
Makadirio ya Kodi taarifa zikiwa nusu ni
Tsh 862,
Makadirio ya Kodi taarifa zikiwa Kamili ni
Tsh 487,000 +5.3% ya kiwango kilichozidi katika 16,000,000.

KODI YA BIASHARA KWA MFANYABIASHARA
ANAETUNZA TAARIFA ZA FEDHA

 Kundi hili hulipa Kodi kutokana na faida wanatoipata .
 Mapato ya mwaka yanazidi Tsh20,000,000.
 Hulazimika kuandaa taarifa ya fedha ya mwaka.
Mchanganuo was Kodi upo Kama ifuatavyo;

UPANDE WA TANZANIA BARA.

Kiwango kinachopaswa kutozwa Kodi kwa mwaka
Mapato ya mwaka yasipozidi 20,400,000.
Hakuna Kodi (-) NIL
Mapato yanapozidi 20,400,000 lakini yakawa sawa au chini ya 4,320,000.

Kiwango Cha Kodi ni 205,200 + 20% ya kiwango kilichozidi katika 4,320,000.
Mapato yanapozidi 6,480,000 lakini yakawa sawa au chini ya 8,640,000
Kiwango Cha Kodi ni 637,200 +25% ya kiwango kilichozidi katika 6,480,000.
Mapato yanapozidi 8,640,000
Kiwango Cha Kodi ni 1,177,200 + 30% ya kiwango kilichozidi katika 8,640,000.

UPANDE WA ZANZIBAR

Mapato ya mwaka yasipozidi 1,800,000.
Kiwango Cha Kodi ni Hakuna (-) NIL
Mapato yakiwa zaidi ya 1,800,000 lakini chini au sawa na 4,320,000.
Kiwango Cha Kodi ni 13% ya kiwango kilichozidi katika 4,320,000.
Mapato yakiwa zaidi ya 4,320,000 lakini chini au sawa na 6,480,000.
Kiwango Cha Kodi ni 327,600 +20% ya kiwango kilichozidi katika 432,000.
Mapato yakiwa zaidi ya 6,480,000 lakini chini au sawa na 8,640,000
Kiwango Cha Kodi ni 759,600 + 25% ya kiwango kilichozidi katika 6,480,000.
Mapato yakiwa zaidi ya 8,640,000.
Kiwango Cha Kodi ni 1,299,600 + 30% ya kiwango kilichozidi katika 8,640,000.

HITIMISHO

 Ni imani yangu katika makala hii fupi umepata mwangaza kiasi fulani katika maswala ya Kodi hususani
katika biashara ndogo ndogo.
 Nakaribisha maoni, nyongeza na marekebisho pale ambapo Kuna kitu umeona taarifa Yale haiko sawa.
 Tukutane katika makala zijazo .

IMEANDALIWA NA

BENSON FLEXON SHIRIMA
MHITIMU CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM SHULE YA BIASHARA .
MWANZILISHI NA MMILIKI WA @CHIKAZI_POINT
EMAIL : bensonflexon@gmail.com
FACEBOOK BENSON FLEXON SHIRIMA
INSTAGRAM @BENITTO_TZ
WATSAP 0654859954
CALL/TXT 0653384656

mr_politicia_rawfed
JF-Expert Member
Joined: Sep 20, 2015
275 101 60

4 minutes ago #2

> Benittotz said: ↑
>
> *ZIFAHAMU AINA ZA KODI NA VIWANGO VYAKE KWA MFANYABIASHARA MDOGO NA WA KATI.*
>
> *: KODI NI NINI?*
>
> *Click to expand...*

Shukrani Boss

.

sa inakuaje maduka mtu unakuta mtaji ni 4m, afu analipa mapato laki 5..

Apo inakua Shida ni nini.. ??

(You must log in or sign up to reply here.)

FACEBOOK

: KODI NI NINI? KODI NI MCHANGO WA LAZIMA KWA SERIKALI..." CLASS="POPUP">

STAFF ONLINE NOW

M Mhariri
Content Quality Controller

 Maxence Melo
JF Founder

FORUM STATISTICS

TOPICS	MEMBERS	POSTS
1,173,982	442,798	27,068,197

FACEBOOK

TWITTER

WHO ARE WE?

JamiiForums is a 'User Generated Content' site; anyone can register (MUST) and comment or start a new topic. You are always welcome!

Read more...

WHERE ARE WE?

We have our offices in Dar es Salaam but we still work virtually. For anything related to this site please Contact us.

Contact Us Now...